Ewe Mwanafunzi wa ‘Ilmu Jitahadhari Usije Ukawa Abu Shibr!

Sheikh Ahmad an-Najjâr [*Hafidhahullâh*]

Ewe Mwanafunzi wa ‘Ilmu Jitahadhari Usije Ukawa Abu Shibr!

Ndugu zangu wapendwa, nimependelea kuangazia ukweli ulio na machungu wa mtu ambaye ni “Abu Shibr”, aliye jeuri wa kupindukia na ambaye ni *Muta’âlim* [mwanafunzi bandia anayejifanya kuwa ana ‘ilmu]. Huu ni uhakika uliotusibu sisi na ambao mpaka sasa hivi unaendelea kutusibu, na ufisadi mwingi na yenye kusababisha ufisadi yalianzia kutoka kwake, yakiandamana vilevile na dhulma juu ya haki za Allaah na haki za wanaadamu.

Kwa bahati mbaya, kwa vile hali hiyo imefichika ikawa haitambuliki na wale waliotumbukia ndani ya janga hilo, njia ya pekee ya kuyazungumzia matukio yake ni kutokana na masimulizi jinsi yanavyojiri na katika kutaja sifa zake. Hawawajibiki kwa lolote isipokuwa watizame iwapo wamekumbwa na mitihani ya sifa zilizotajwa au ukweli uliosambazwa au kinyume chake. Iwapo mtu atajikuta yakwamba ametumbukia kwenye mojawapo ya sifa hizo basi itampasa ajitahidi kujiepusha mahali hapo na ajue hadhi yake ya uhakika na asidanganyike kwa idadi kubwa ya wajinga ambao ni wenye kumsifu yeye. Huu ndio ukweli niliotaka kuwasimulia, na sifa nilizokusudia kuwatajia ni;

Ewe Mwanafunzi wa ‘Ilmu Jitahadhari Usije Ukawa Abu Shibr!

Yakwamba baadhi ya wenye kutafuta ‘ilmu hukusudia tu kuhifadhi matamshi ya yoyote ambaye wao humsifu kupita kiyasi na dalili zake, ufahamu wake hata haupiti chochote Zaidi ya hiki, lakini akadhani yakuwa ameipata ‘ilmu nzima iliyokamilika au sehemu yake kubwa. Anadhani yakwamba ana uwezo wa kutafautisha baina ya haki na bâtil, na afanyapo hivyo husababisha matatizo mengi kwa watu, kwa vile kutegemea juu ya hayo kunawajibisha watu wakubali rai moja kwa vile mwanafunzi huyu wa ‘ilmu-bandia hana la Zaidi ajualo. Huwenda pakazuka utwi’ifu na makanusho kutokana na haya ambapo yoyote atakaekuwa na rai inayokhitilafiana ataanza kuchukiwa, asusiwe na kuvunjiwa hadhi yake, na haya ndiyo yenye kutokea. *Miskîn* huyu hazingatii yakwamba kuna rai nyengine katika mas’ala iliyo kinyume cha rai ya Sheikh wake, kama asivyojua kuhusu misingi yenyewe ya rai hizo, sababu zake za kitaalamu, msingi wake, vipingamizi vyake na jawabu zake; *na kadhaalika*. Huwenda akazijua baadhi yake lakini nyengine asizijue, na kutokana na hivyo akadhulumu kutokana na ajuavyo, na ukweli wa mambo ni kwamba makosa yake ni mengi kuliko mapato yake, na utambuzi wake katika mas’ala na matamshi ni utambuzi mchache tu, yaani hata lau kama itasemekana kuwa ni utambuzi. Kutokana na jeuri zake na udanganyifu utamkuta kazi yake ni kutia pua yake katika [ataka kunusa] kila kitu, kwahiyo anasababisha madhara zaidi kuliko anavyonufaisha.

Jambo la hatari katika mas’ala ya ‘ilmu na watu wake ni: Wanafunzi waendelee kudumisha uadilifu iwapo daraja zao zitafanyiwa dhulma. Hili ni suala linalotusibu mno, na lau kama mtu atatosheka na kile anachokijua tu na akajijua kiwango cha nafsi yake, basi ufisadi na kuusababisha huo ufisadi hakutotokana na yeye. Lakini hata hivyo kwa bahati mbaya wao huvuka mipaka isipokuwa kwa wale waliorehemewa na Allâh. Wengi wao daima utawakuta wakiranga kutoka kwenye rai hii mpaka kwenye rai ile, na yoyote aliyekuwa ni mzuri jana amegeuka na kuwa mbaya leo na kuendelea kama hivyo. Twamuomba Allâh atuhifadhi kutokamana na usaliti wa kiyasi hicho. Na miongoni mwao ni wale waliosoma kwa wanavyuoni, lakini hatahivyo hawana msingi mzuri kisawasawa; na miongoni mwao ni wale waliojisomesha kutokamana na vitabu na usajili wa sauti pasi na kuchukuwa moja kwa moja kutoka kwa wanavyuoni, hii haimaanishi yakwamba wote ambao hawakuchukuwa ‘ilmu moja kwa moja kutoka kwenye mikono ya wanavyuoni kuwa ni madhaifu au hawana misingi mizuri, lakini mafunzo hupatikana katika adabu za usomaji kama huo na kuandama njia ya sawa katika kutafuta ‘ilmu. Kabla ya yote hayo ni kwamba kufaulu kunatokamana na Allâh.

Katika sababu za jeuri kama hizo na kiburi kuhusiana na ‘ilmu ni haya yafuatayo:

1) Kuwa na misingi dhaifu yakipatikana kwa mwanafunzi bandia anayejifanya kwa jeuri kuwa amehitimu kiwango cha juu cha ‘ilmu.
2) Wajinga katika kumsifu na kumrufaisha kupita daraja anayostahiki.
3) Ujeuri wake anapozungumzia kuhusiana na jambo asilokuwa na ‘ilmu nalo.

Tiba ya maradhi hayo ni; Anapaswa mtu kutambua kiwango chake cha daraja aliyo nayo, wala asidanganyike kwa sifa za watu wajinga jinsi wanavyomsifu nazo, na wanafunzi waaminifu wenye ‘ilmu wambainishie daraja yake katika ‘ilmu, na wapitie

njia za naswaha na mawaidha mema katika kumkosoa ili kiwango chake cha uhakika kipate kujulikana. Hatimae, yaliyonihamasisha mimi mpaka nikaandika haya ni kuwaamsha [watu] hao na kuwabainishia yakwamba kuyatilia uzani hao wanayoandika hayako kwenye mikono ya watu wajinga, bali yako kwa wanafunzi imara wenye ‘ilmu. Vilevile, kwa kuandika makala haya sikumkusudia mtu fulani makhsusi, bali lengo langu ni kuzibainisha tabia kwa ujumla bila ya kuzikusudia kumuhusisha mtu fulani. Nauwacha ubainifu huu kwa wanafunzi imara wenye ‘ilmu. *Tahqîqul Manât* [ubainifu wa hukmu], kwa njia ya kuzitaja shahada na kuthibitisha ufafanuzi ili wanafunzi imara wenye ‘ilmu wenye kuujuwa ukweli wa mwenye kujitangazia madai yake, kwani ni wangapi wenye kujidai walioko ambao kazi zao ni kuwahadaa wajinga. Kwa hakika wengi hudai yakwamba wana ‘ilmu na kwamba wameipata, lakini ‘ilmu yenyewe haiwatokei wao ushahidi. Allâhul Musta’ân.

Namuomba Allâh atuja’aliye kufuzu katika kila la kheri na atuongoze.

Muandishi’

Dr. Ahmad Muhammad as-Sādiq an-Najjār
14th Dhu’l-Hijjah 1436 AH

Kwa Hisani ya brixtonmasjid.co.uk

http://brixtonmasjid.co.uk/project/9147/

http://www.alngar.com/user/Re_article.aspx?id=7112

Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad.